

## TANGAZO KWA UMIMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMILAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJII WA MPWAPWA (“Mpwapwa WSSA”) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

**Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-016**

Mnamo tarehe 3 Julai 2018, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Mpwapwa (Mpwapwa WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Jedwali namba 1 hadi 4 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

#### Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Aina za Wateja	Matumizi (M3)	Bei za Sasa	Bei zilizopendekezwa					
			2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko
Majumbani	0-10	630	45%	1,520	31%	1,990	24%	2,460
	<10	1,045						
Taasisi	0-10	1,285	30%	2,040	23%	2,510	19%	2,990
	<10	1,565						
Biashara	0-10	1,325	30%	2,080	20%	2,490	16%	2,890
	<10	1,605						
Taasisi za kidini	1	1,285	37%	1,760	27%	2,230	21%	2,700
Magati		2,100	200%	3,000	0%	3,000	0%	3,000
Viwandani		NA	NA	2,080	20%	2,490	16%	2,890

**Jedwali 2: Gharama ya Huduma ya Sasa na Iliyopendekezwa (Shilingi/mwezi)**

Aina za Wateja	Bei za sasa	Tozo zilizopendekezwa kwa miaka mitatu			
		2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	2,500		0	0	0
Taasisi	4,000		0	0	0
Biashara	4,000		0	0	0
Taasisi za Kidini	3,000		0	0	0
Viwandani	4,000		0	0	0

**Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)**

Aina za Wateja	Bei za sasa	Badiliko	Tozo zilizopendekezwa				
			2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa
Biashara							
Taasisi							
Viwandani							

**Jedwali 4: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)**

Aina za Wateja	Bei za sasa	Tozo Zinazopendekezwa					
		2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko
Majumbani	15,000	33%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Taasisi	20,000	25%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Biashara	20,000	25%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Taasisi za Dini	20,000	0%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Viwandani	20,000	25%	25,000	0%	25,000	0%	25,000

Kutokana na wasilisho la Mpwapwa WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kuongeza mapato ili kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo, na kuweza kupata fedha za kuboresha na kulipia uchakavu wa miundombinu ya majisafi.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 13 Septemba, 2018, katika Jumba la Maendeleo, Mpwapwa Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa

ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **18 Septemba, 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au ofisi za Mpwapwa WSSA zilizoko mjini Mpwapwa.

**Imetolewa na  
Kaimu Mkurugenzi Mkuu  
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)  
24 August 2018**